

**HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA N A S H E R I A M H E S H I M I W A DKT.  
ASHA-ROSE MIGIRO, (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO  
YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

**A. UTANGULIZI**

- 1.** *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016.
- 2.** *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Kwa namna ya pekee napenda kutoa asante nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuendelea kulitumikia taifa letu katika ngazi hii ya uongozi.
- 3.** *Mheshimiwa Spika*, kwa masikitiko makubwa napenda kutoa salamu za pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi kwa kuondokewa na Mbunge wao Kapteni John Damiano Komba, aliyefariki tarehe 28.02.2015. Hakika mchango wake utakuwa na nafasi ya pekee katika historia ya jimbo lake. Hali kadhalika Watanzania wengi tutaendelea kumkumbuka kama askari shupavu wa mstari wa mbele na mhamasishaji wa aina yake katika kukuza umoja na utangamano wa taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Kapteni John Damiano Komba mahali pema peponi, amina.
- 4.** *Mheshimiwa Spika*, naomba sasa uniruhusu nikupongeze wewe, Mheshimiwa, kwa kuliongoza Bunge letu kwa umahiri, ushupavu na weledi mkubwa. Uongozi wako umeliweka Bunge letu katika ramani ya dunia na kufanya wewe, Mheshimiwa, ukabidhiwe nafasi mbali mbali za uongozi ndani na nje ya bara letu, na hivi karibuni kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC). Vile vile nimpongeze Naibu Spika, Mhe. Job

Ndugai, mbunge wa Kongwa na wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wao mahiri kila wanapokalia kitu cha Spika.

**5. *Mheshimiwa Spika*,** naomba kwa dhati nimpongeze Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki, na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa dira na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**6. *Mheshimiwa Spika*,** napenda hali kadhalika, kumpongeza Mheshimiwa Jason Samson Rweikiza, mbunge wa Bukoba Vijiji, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Wizara yetu inayo imani kubwa kwake binafsi na kwa Kamati anayoiongoza. Katika muktadha huo, Wizara yetu inatoa shukrani nyingi kwa Kamati yake, kwa ushauri mzuri na mapendeleko ambayo yamesaidia sana kuboresha Mpango na Makadirio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Ninaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana na Kamati hii ili kutuwezesha kufikia dira ya Wizara ya *Haki Sawa kwa Wote na kwa Wakati*, pamoja na Dira ya Taifa kuelekea mwaka 2025.

**7. *Mheshimiwa Spika*,** ninayo furaha kuwapongeza Waheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja, na Innocent Rwabushaija Sebba, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, kuwa wabunge. Ninawatachia kheri na mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

**8. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara ya Katiba na Sheria inazo taasisi, ofisi na idara ambazo zinafanya kazi chini ya mwamvuli wake. Hizi ni Mahakama ya Tanzania; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Tume ya Kurekebisha Sheria; Tume ya Utumishi wa Mahakama; Wakala wa Usajili, Ufilisi, na Udhamini; Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; na Chuo cha Uongozi wa Mahakama.

**9. *Mheshimiwa Spika*,** kwa kuongozwa na Dira ya Wizara ya *Haki Sawa kwa Wote na kwa Wakati*, Wizara imejipanga vema kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake makuu ambayo ni pamoja na masuala ya Katiba; kusimamia sheria na utoaji haki; kuandaa miswada ya

Sheria; kuendesha mashtaka; kutoa ushauri wa kisheria na kuendesha mashauri ya madai; kukuza na kuhifadhi haki za binadamu; kushughulikia usajili, ufilisi na udhamini; kushirikiana kimataifa katika kubadilishana wahalifu; kutoa mafunzo ya uanasheria na kusimamia ustawi na maendeleo ya watumishi wake.

## **B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**10. Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nifanye mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Katika kipindi hiki, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 234,246,819,000. Kati ya hizo, shilingi 48,804,234,000 ni mishahara, shilingi 131,880,015,000 ni kwa matumizi mengineyo na shilingi 53,562,570,000 ni fedha za maendeleo. Kufikia Aprili, 2015 fedha zilizopokelewa ni jumla ya shilingi 108,903,009,746 ambapo kati ya hizo shilingi 42,898,115,751 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 64,852,164,777 ni matumizi mengineyo na shilingi 1,152,729,218 zikiwa ni fedha za maendeleo za nje. Fedha zote zilizopokelewa ni sawa na asilimia 46.5 ya bajeti iliyoidhinishwa.

**11. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mpango kazi wa mwaka 2014/2015, Wizara ilitumia fedha zilizopokelewa kutekeleza vipaumbele vyake kama ifuatavyo: kusimamia mchakato wa mabadiliko ya Katiba; kuimarisha mfumo wa sheria na misingi ya utoaji haki; kusimamia na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora; kuimarisha usajili wa matukio muhimu ya binadamu; kutoa ushauri na huduma za kisheria; na kuimarisha uwezo wake wa kitaasisi. Vipaumbele vyta Wizara vinatokana na dhima ya Wizara ya kukuza utawala wa sheria, haki na usawa kwa kutoa huduma bora za kisheria. Naomba kulieleza Bunge lako tukufu kwamba tumeweza kufanya yote haya tukiongozwa na kauli mbiu isemayo: *haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyopokonywa.*

## **MCHAKATO WA MABADILIKO YA KATIBA**

**12. Mheshimiwa Spika**, Bunge Maalum la Katiba lilihitimisha jukumu lake tarehe 4 Oktoba, 2014 na kukabidhi Katiba Inayopendekezwa kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa

Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, tarehe 8 Oktoba, 2014 mjini Dodoma. Kufuatia tukio hilo la kihistoria, Wizara ilichapisha nakala 2,000,400 za Katiba Inayopendekezwa. Kati ya hizo, nakala 2,000,000 zilichapishwa katika mfumo wa maandishi ya kawaida, nakala 200 zilichapishwa katika maandishi ya nukta nundu kwa ajili ya watu wasioona, na nakala nyingine 200 zilichapishwa katika maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya watu wenye ualbino. Nakala 1,141,300 zilizo katika maandishi ya kawaida zilisambazwa kwa wananchi Tanzania Bara ambapo kila kata ilipata nakala 300; na nakala 200,000 zilipelekwa Zanzibar. Nakala 658,700 zilisambazwa kwa Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali, vyama vyasiasa, jumuiya za kidini, taasisi za elimu ya juu na asasi za kiraia Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

**13. *Mheshimiwa Spika*,** kusambazwa kwa Katiba Inayopendekezwa kumesaidia sana kujenga uelewa wa maudhui ya Katiba Inayopendekezwa ili kuwawezesha wananchi kijiandaa kwa kura ya maoni wakati utakapofika. Napenda kutoa rai kwa viongozi wa Serikali, vyama vyasiasa, jumuiya za kidini, asasi za kiraia na wanajamii kwa ujumla kuwahamasisha wananchi kuisoma Katiba Inayopendekezwa na kuilewa vizuri kwa manufaa ya taifa letu.

## **MFUMO WA SHERIA NA UTOAJI HAKI**

### **Uendeshaji wa Mashauri na Utoaji Haki**

**14. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ilimarisha usikilizaji wa mashauri yaliyosajiliwa mahakamani na kupunguza idadi ya mashauri ya muda mrefu katika ngazi zote za mahakama. Katika kipindi hicho kulikuwa na jumla ya mashauri 247,267 ambapo mashauri 70,484 ni ya kutoka mwaka 2013/2014; na mashauri 176,783 ni yaliyosajiliwa mwaka 2014/2015. Kati ya yote hayo, jumla ya mashauri 179,469 yalisikilizwa na kutolewa uamuza.

**15. *Mheshimiwa Spika*,** Kamati za Kusukuma Uendeshaji Mashauri (*case-flow management committees*) ambazo zipo katika ngazi za wilaya, mkoa, kanda na taifa, zimekuwa nyenzo muhimu katika kupunguza idadi ya mashauri ya muda mrefu na msongamano na mahabusu. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliratibu vikao vyaa Kamati hizi katika ngazi mbalimbali pamoja na kuyatembelea maeneo wanamoshikiliwa watuhumiwa wa uhalifu ili kusikiliza kero zao. Wizara itaendelea kuziimarisha Kamati hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi kwa kuzingatia ratiba za vikao, kanuni na taratibu nyingine zilizowekwa.

**16. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka unaokwisha wa fedha, Wizara ilisimamia utekelezaji wa Mpango wa Kutenganisha Mashtaka na Upelelezi (*civilianization of prosecutions*). Madhumuni ya mpango huu ni kudhibiti, kusimamia uendeshaji wa mashtaka na kuratibu shughuli za upelelezi kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa kuzingatia misingi ya sheria. Kupitia mpango huu mashauri ya jinai katika mahakama za wilaya na mahakama za hakimu mkazi yanaendeshwa na mawakili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mpango huu umekuwa ni kiungo muhimu kati ya Wizara na vyombo vyta upelelezi wa makosa ya jinai katika kuharakisha upatikanaji haki na kuongeza ufanisi.

**17. *Mheshimiwa Spika*,** madhumuni mengine ya kuanzishwa kwa mpango wa kutenganisha mashtaka na upelelezi ni kuhakikisha huduma za uendeshaji mashtaka zinapatikana karibu na jamii. Hivyo, Wizara imefanikiwa kufungua ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mikoa yote ya Tanzania Bara na inakusudia kufikisha huduma hizo kwenye ngazi ya wilaya nchini kote kwa kuanzia na wilaya za Monduli na Temeke.

**18. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka wa fedha, 2014/2015 Wizara ilisimamia uendeshaji wa mashauri ya jinai 8,025 katika ngazi za mahakama ya rufani, mahakama kuu: mahakama za hakimu mkazi; na mahakama za wilaya. Kati ya hayo, mashauri 5,772 yalihitimishwa, na mengine 2,253 yanaendelea kusikilizwa.. Aidha, Wizara iliratibu uendeshaji wa Jukwaa la Taifa la Haki Jinai na kushirikiana na vyombo mbali mbali vinavyohusika na masuala ya sheria ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika sekta hii ya haki jinai. Jukwaa hili liliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka, na. 27 ya mwaka 2008, na linashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wakuu wa taasisi zinazohusika na uchunguzi wa makosa, uendeshaji na usimamizi wa makosa ya jinai.

**19. *Mheshimiwa Spika*,** vitendo vya rushwa na udanganyifu, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevyia vimekuwa tishio katika jamii. Kadhalika, vitendo vya mauaji na ukatili kwa watu wenye ualbino vimelifiedhehesha sana taifa na kuchafua taswira ya nchi yetu. Wakati Bunge lako tukufu likiendelea, tarehe 13 Mei, 2015 mwanamke mmoja katika wilaya ya Mlele, mikoa wa Katavi, alikatwa kiganja cha mkono kwa imani za kishirikina. Wizara yetu imejizatiti

kukabiliana na matukio haya kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa sekta ya sheria na waliomo ndani ya jamii.

**20. Mheshimiwa Spika**, kwa mnasaba huo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilisimamia uendeshaji wa mashauri 14 ya mauaji na ukatili kwa watu wenye ualbino. Kati ya hayo, shauri moja lilihitimishwa ambapo watuhumiwa wanne walipatikana na hatia ya mauaji na kupewa adhabu ya kifo; mashauri sita yako katika hatua mbalimbali za usikilizaji mahakamani, na mashauri saba yako katika hatua ya upelelezi.

**21. Mheshimiwa Spika**,`niruhusu nitumie fursa hii kutoa mwito maalum kwa Watanzania wote kuchukua hatua za dhati kukomesha vitendo hivi vya kikatili, vya kijinai, vinavyoikiuka haki za binadamu na vinavyochafua jina zuri la nchi yetu. Ni sharti tutambue kwamba **maisha ya watu wenye ualbino ni maisha yetu – tuyalinde!**

**22. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa dawa za kulevya, katika mwaka wa fedha 2014/2015 kulikuwa na jumla ya mashauri 79 yaliyohusu dawa za kulevya aina ya *heroine, cocaine na cannabis*. Kati ya hayo, mashauri 58 ni ya zamani na 21 ni mapya. Mashauri yote haya yapo katika hatua mbalimbali ya kusikilizwa. (**Kiambatisho A**)

**23. Mheshimiwa Spika**, Wizara, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kufuatilia na kuchukua hatua za kisheria kwa watu watakaobainika kujihusisha na dawa za kulevya. Katika kukabiliana na tatizo hili Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali katika vita hivi wakiwemo wananchi wenyewe, viongozi wa kisiasa, wa kidini na wa kijamii.

**24. Mheshimiwa Spika**, kwa mashauri yanayohusu rushwa na udanganyifu, kulikuwa na majalada 250 yaliyopokelewa na Mkurugenzi wa Mashtaka kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Baada ya kufanyiwa uchambuzi, majalada 131 yaliandaliwa hati za mashtaka na 72 yalirejeshwa TAKUKURU kwa uchunguzi zaidi. Majalada 47 yaliyobaki yanaendelea kufanyiwa uchambuzi.

**25. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliwakilisha Serikali mahakamani katika mashauri 839 yanayoihusu, ndani na nje ya nchi. Mashauri hayo ni ya

kikatiba, madai, na yale yanayohusu ukiukwaji wa haki za binadamu. Kati ya hayo, mashauri 37 yalihitimishwa na 802 yako katika hatua mbalimbali za kusikilizwa.

**26. *Mheshimiwa Spika*,** kuhusu mashauri ya kikatiba, Wizara iliiwakilisha Serikali katika mashauri 93 ambapo mashauri matano yalihitimishwa na mengine 88 yanaendelea kusikilizwa. Mashauri ya madai yalikuwa 51 na yote yanaendelea kusikilizwa. Vilevile, Wizara iliiwakilisha Serikali katika mashauri sita ya ukiukwaji wa haki za binadamu yanayoendelea kusikilizwa katika Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliyoko Banjul, Gambia.

#### **Utafiti, Urekebu na Uandishi wa Sheria**

**27. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imechukua hatua za mara kwa mara kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mfumo imara wa sheria unaokidhi mahitaji ya jamii kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ili kufanikisha hilo, Wizara iliendesha tafiti mbalimbali ambazo zimekuwa msingi wa marekebisho ya baadhi ya sheria na kutungwa kwa sheria mpya. Tafiti hizo zinahusu sheria za huduma za kijamii kwa wazee; sheria zinazolinda haki za watumiaji wa bidhaa na huduma; na sheria zinazosimamia haki jinai. Vile vile, Wizara ilichambua hukumu 70 za Mahakama ya Rufani kwa lengo la kupata misingi ya kisheria iliyotumika katika hukumu hizo ili kusaidia marekebisho ya sheria mbalimbali. Wizara pia ilishirikiana na wadau wengine katika kuwianisha sheria za nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki ili kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo.

**28. *Mheshimiwa Spika*,** matokeo ya tafiti zilizofanyika ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa wa mwaka 2015 ambao umesomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika mkutano wa 19 wa Bunge, mapendekezo ya kutunga Sheria ya Msaada wa Kisheria na mapendekezo ya kutunga Sheria ya Kulinda Watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi. Hivi sasa mapendekezo hayo yapo katika mchakato wa kiserikali wa kuyafanya uamuzi.

**29. *Mheshimiwa Spika*,** uandishi na uwasilishaji wa miswada ya sheria Bungeni ni moja ya hatua muhimu katika kuimarisha utawala wa sheria nchini. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilianda jumla ya miswada 21 iliyosomwa mbele ya Bunge lako ambapo miswada 14 kati ya hiyo ilijadiliwa na kuitishwa na Bunge. Miswada yote iliwasilishwa Bungeni kwa Kingereza na Kiswahili ili kuzifanya sheria hizi zieleweke kwa urahisi na

wananchi. Vile vile, Wizara ilihakiki sheria ndogo 286 na kuzitangaza katika Gazeti la Serikali. Sheria 128 zilifanyiwa urekebu katika kipindi hichi.

**30. *Mheshimiwa Spika*,** sambamba na kuhakikisha kuwa miswada yote ya sheria inaandikwa kwa Kiingereza na Kiswahili, Wizara ilitafsiri sheria nyingine za nchi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Sheria zilizotafsiriwa ni Sheria ya Ushirikiano wa Pamoja wa Kimataifa Katika Masuala ya Jinai, Sura ya 254; Sheria ya Silaha na Risasi, Sura ya 223; Sheria ya Kuhamisha Wafungwa ya mwaka 2004; Sheria ya Uangalizi wa Wahalifu, Sura ya 247; na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Serikali, Sura ya 5.

## **MIFUMO YA UTOAJI HUDUMA**

**31. *Mheshimiwa Spika*,** uhakika na ubora wa huduma za kisheria zinazotolewa na Wizara unategemea sana kuwepo kwa miundombinu imara kama vile majengo, vitendea kazi vyta kisasa na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Hivyo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilitekeleza miradi mbalimbali ili kuimarisha upatikanaji wa majengo ya ofisi, nyumba za watumishi na matumizi ya TEHAMA.

**32. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara ilitumia TEHAMA katika usikilizaji wa mashauri, upokeaji na uchambuzi wa malalamiko yaliyohusu kuvunjwa kwa haki za binadamu na kukiukwa kwa misingi ya utawala bora; na ufuatiliaji wa majalada ya mashauri ya jinai. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara inaendelea kukamilisha maandalizi ya kuanzisha mfumo wa malipo ya ada za usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini kwa njia ya kielektroniki. Mifumo hii itasaidia kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

**33. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilikuwa na miradi ya ujenzi wa jengo la Mahakama ya Tanzania, Dar es Salaam; ujenzi wa nyumba 12 za majaji katika mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Dodoma, Iringa, Tanga, Arusha, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mtwara na Kilimanjaro; ujenzi wa Mahakama Kuu katika mikoa ya Shinyanga Kigoma, Lindi, Manyara, Mara, Morogoro, na Singida; ujenzi wa Mahakama 9 za wilaya za

Bagamoyo, Baridadi, Bunda, Bukombe, Hanang, Kasulu, Kilindi, Nkasi, Makete; na ujenzi wa Mahakama 26 za Mwanza nchini.

**34. *Mheshimiwa Spika*,** vile vile, Wizara ilikuwa na miradi ya ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Tabora, Mwanza, Ruvuma na Mbeya; Mahakama 8 za Hakimu Mkazi katika Mikoa ya Singida, Mara, Ruvuma, Tabora, Kigoma, Rukwa, Kagera na Morogoro. Vile vile ilikuwa na miradi ya ukarabati wa majengo ya Mahakama 4 za wilaya za Monduli, Kiteto, Newala na Muleba; na mahakama tisa za mwanzo za Magugu (Babati), Vwawa (Mbozi), Lindi Mjini, Kiteto, Bereko (Kondoa), Robanda (Serengeti), Gairo, Rusumo (Ngara), na Makambako. Miradi yote ya ujenzi na ukarabati iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji, (**Kiambatisho B**).

**35. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarisha utendaji kazi wa Mahakama ya Tanzania, Rais alifanya uteuzi wa majaji wawili wa Mahakama ya Rufani, Jaji Kiongozi na majaji 20 wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Kati ya majaji walioteuliwa tisa ni wanawake na 13 ni wanaume. Pia, Rais alifanya uteuzi wa Msajili wa Mahakama ya Rufani na Msajili wa Mahakama Kuu. Katika kipindi hicho walajiriwa mahakimu wakaazi 57 na wasimamizi wa mahakama (court administrators) 24. Pia, Wizara iliendesha programu za mafunzo kwa Kamati za Maadili za mikoa na wilaya ili kuimarisha nidhamu kwa watumishi wa mahakama.

**36. *Mheshimiwa Spika*,** Kamati hizi za mikoa na wilaya zimekuwa vyombo muhimu vya kusimamia maadili na nidhamu za watumishi wa mahakama. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliziwezesha Kamati saba za mikoa na 36 za wilaya kuendesha vikao vya kuchunguza na kujadili malalamiko ya ukiukwaji wa maadili ya mahakimu. Pia, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilishughulikia mashauri 27 ya nidhamu na kuyatolea uamuzi. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa Kamati za Maadili za mikoa ya Dodoma, Katavi, Rukwa na Singida ili ziweze kutekeleza majukumu yake vizuri.

## **HAKI ZA BINADAMU NA ELIMU KWA UMMA**

**37. *Mheshimiwa Spika*,** mpango wa elimu kwa umma ni mkakati muhimu wa Wizara wa kuhakikisha watu wanafahamu na kudai haki zao; na wanajua wajibu wao kwa mamlaka za nchi.

Katika kutekeleza mpango huo, Wizara ilirusha hewani vipindi 25 vya redio na televisheni na kusambaza machapisho 15, 500 ya aina mbalimbali kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara, maonesho ya kitaifa, idara na taasisi za serikali. Vile vile, Wizara ilifanya mikutano na viongozi wa kijamii na watendaji wa Serikali katika wilaya za Chato na Tabora ili kuongeza uelewa wa wajibu wao wa kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu.

**38. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu, Wizara ilitoa elimu kwa wafanyakazi wa viwanda vilivyo chini ya mradi wa Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa za Kuza Nje (EPZA) katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga. Jumla ya wafanyakazi 884 kutoka viwanda 14 walishiriki mafunzo hayo, kati yao wanawake walikuwa 389 na wanaume 495. Vile vile, Wizara iliratibu na kusimamia maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Ulimwenguni yaliyofanyika tarehe 10 Desemba, 2014 na ilitumia fursa hiyo kueleza juhudini zinazofanywa na Serikali katika kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu chini ya mfumo wa Umoja wa Mataifa wa mapitio kwa kipindi maalum (*universal periodic review mechanism*).

**39. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara iliiwakilisha Serikali kwenye mikutano mbali mbali nje ya nchi ambayo ilisaidia kubadilishana uzoefu na mataifa mengine, kuimarisha utendaji na kuongeza ufanisi kazini. Mikutano hiyo ni pamoja na mkutano wa Umoja wa Afrika kuhusu haki za kijamii na kiuchumi uliofanyika Ghana; na mkutano uliojadili Demokrasia, Utawala Bora na Uchaguzi uliofanyika nchini Ethiopia.

## **USAJILI, UFILISI NA UDHAMINI**

**40. *Mheshimiwa Spika*,** usajili wa matukio muhimu ya binadamu una manufaa kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa takwimu zinahotijika katika mipango ya maendeleo; na kuweka mazingira mazuri ya kuimarisha haki mbalimbali za raia. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilitekeleza mikakati ya jumla na mahsusini ya kuimarisha usajili wa matukio yanayomhusu binadamu kama vile hali ya ndoa, talaka, vizazi na vifo. Kupitia mikakati ya jumla Wizara ilisajili vizazi 349,440; vifo 49,168; ndoa 11,351 talaka 118 na watoto 34 walioasiliwa.

**41. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilianda programu mahsusini ya usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano iliyotekelizwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Chini ya programu hii, Wizara ilisajili jumla ya watoto 59,463 na kutoa vyeti vya kuzaliwa bila malipo. Mkakati mwingine mahsusini ulikuwa ni usajili wa watoto waliopo mashulenii waliokuwa na umri wa kati ya miaka 6 na 18 ambapo Wizara ilisajili jumla ya watoto 18,800.

**42. Mheshimiwa Spika,** kutokana na jitihada zinazochukuliwa, Wizara imeweza kuongeza kiwango cha usajili kutoka wastani wa chini ya asilimia 10 mwaka 2012 hadi asilimia 16 ilipofika Aprili 2015. Hata hivyo, kiwango hiki bado ni cha chini ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2020. Hivyo, Wizara ilifanya tathmini ya mfumo uliopo wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu na kuandaa Mkakati wa Taifa ili kuimarisha shughuli za usajili.

**43. Mheshimiwa Spika,** sanjari na shughuli za usajili Wizara ilitoa hati 203 kwa wadhamini wa taasisi na asasi za kijamii na kuwapa elimu juu ya haki na wajibu wao wa kisheria kulingana na Katiba za asasi wanazozisimamia. Aidha, Wizara ilitoa elimu kwa umma kuhusu mirathi, namna ya kuandika na kuhifadhi wosia kuitia redio, televisheni na mabaraza ya wafanyakazi.

## **USHAURI NA HUDUMA ZA KISHERIA**

### **Ushauri na Majadiliano ya Mikataba**

**44. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ilitoa ushauri wa kisheria katika maeneo mbalimbali. Wizara ilihakiki na kuchambua mikataba 2,993 ya kibiashara, ununuzi wa umma na uwekezaji. Pia, Wizara ilitoa ushauri wa kisheria kwa masuala anuwai yaliyowasilishwa kwake na wizara, idara, wakala na taasisi nyingine za umma.

### **Huduma ya Msaada wa Kisheria**

**45. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuiwakilisha Serikali katika masuala ya kisheria, Wizara ilitoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi wasio na uwezo wa kupata huduma za uwakili kupitia mfumo wa kawaida uliopo. Huduma zilizotolewa zilihusu elimu na ushauri wa kisheria; na kuandaa nyaraka za kupeleka mashauri mahakamani. Aidha, Wizara ilikamilisha maandalizi ya mapendekezo ya kutunga Sheria ya Msaada wa Kisheria ili kuiwezesha Serikali kusimamia ubora na upatikanaji wa huduma za kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za uwakili nchini.

## **UWEZO WA KITAASISI**

### **Hali ya Watumishi**

**46. Mheshimiwa Spika**, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la mahitaji ya huduma zinazotolewa na Wizara linaloenda sanjari na mahitaji zaidi ya watumishi. Hivyo, Wizara imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kukidhi mahitaji ya watumishi kila yanapojitokeza ambapo katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilipewa kibali cha kuajiri watumishi wapya 460. Pia, katika kipindi hicho watumishi 1,048 walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji wakiwemo 442 wa mafunzo ya muda mfupi, na 606 wa mafunzo ya muda mrefu.

### **Maduhuli ya Serikali**

**47. Mheshimiwa Spika**, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali katika mwaka wa fedha 2014/2015 ni Shilingi 8,571,209,121. Katika kipindi hicho Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi 8,581,417,819 ikiwa ni asilimia 0.12 juu ya makadirio ya awali. Ongezeko hilo linatokana na kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji ada za huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi za Wizara. Kuimarika kwa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali ni chachu kwa Wizara na taasisi zake katika kuboresha huduma zinazotolewa, (**Kiambatisho C**).

## **URATIBU WA TAASISI ZA MAFUNZO**

**48. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ni nyenzo muhimu ya kupata watumishi wenye sifa na kudhibiti ubora wa huduma zinazotolewa. Kwa hiyo Wizara

ilichukua hatua mbalimbali kuiwezesha Taasisi hii kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwa mwaka. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza bajeti ya taasisi kwa asilimia 20 na kuajiri watumishi wapya. Sanjari na jitihada hizo Wizara ilishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kuanzisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuruhusu wanafunzi wa Taasisi kupata mikopo inayotolewa na Bodi hiyo. Katika kipindi hicho Taasisi ilidahili wanafunzi wapya 1,049; na wanafunzi 446 walihitimu masomo yao na kuwa na sifa za kusajiliwa kuwa mawakili, (**Kiambatisho D**).

**49. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Chuo cha Uongozi wa Mahakama (ikiwemo Kampasi ya Mwanza), kilidahili jumla ya wanafunzi 834 kati yao wanafunzi 354 walikuwa katika ngazi ya Cheti cha Sheria na 480 wa Stashahada ya Sheria. Pia, wanafunzi 649 walihitimu masomo yao wakiwemo wanafunzi 386 wa Stashahada na 263 wa Cheti cha Sheria. Udahili na kuhitimu kwa wanafuzi katika Chuo hiki ni hatua muhimu za kukidhi mahitaji ya wataalam wa sheria katika taifa letu, hatua ambazo zitaimarishwa kwa mwaka 2015/16.

### **C. CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO**

**50. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio tuliyoyaeleza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2014/15, changamoto zilizojitokeza ni upungufu wa watumishi, ufinyu wa bajeti ya Serikali, uhaba wa majengo na vitendea kazi. Licha ya changamoto hizi Wizara imefanya jitihada za kuongeza watumishi kila fursa ya kufanya hivyo ilipojitokeza na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo. Aidha, Wizara imeanza kufanya mawasiliano na wawekezaji wa sekta binafsi ili waweze kushiriki katika miradi ya mbalimbali ya maendeleo.

**51. Mheshimiwa Spika**, mkakati mwengine wa kukabiliana na changamoto za kibajeti ni Wizara kuchagua maeneo machache ya kipaumbele na kuhakikisha tija zaidi kwa fedha kidogo zinazopatikana.

### **D. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016**

**52. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itaimarisha huduma zake ili kwenda sambamba na Dhima ya Wizara ya kukuza utawala wa sheria, haki na usawa kwa

kutoa huduma bora na kwa wakati. Ili kufikia azma hiyo Wizara itaelekeza rasilimali zake katika maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni mabadiliko ya Katiba; mfumo wa sheria na utoaji haki; hifadhi ya haki za binadamu na utawala bora; usajili wa matukio muhimu ya binadamu; ushauri wa kisheria na kuiwakilisha Serikali katika masuala ya kisheria; na kuimarisha mifumo ya kitaasisi.

**53. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itasimamia mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Hali kadhalika Wizara itaratibu hatua za kuundwa kwa Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Masharti Yatokanayo na Masharti ya Mpito.

**54. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara itachukua hatua madhubuti za kuimarisha mfumo wa Sheria na utoaji haki kwa kukamilisha utungwaji wa sera ya sekta ya sheria; Sheria ya Mawakili na Sheria ya Ufilisi. Aidha, Wizara itafanya mapitio na utafiti wa sheria zinazoratibu utoaji wa huduma kwa wazee; sheria zinazolinda haki za watumiaji wa bidhaa na huduma; na sheria zinazosimamia mfumo wa haki jinai. Pia, Wizara itasimamia uandishi na urekebu wa sheria mbalimbali, kutayarisha miswada ya sheria kwa Kiingereza na Kiswahili, kupitia sheria mbalimbali ili kuziwianisha na misingi iliyoinishwa na Katiba, na kuridhia maazimio na mikataba mbalimbali ya kimataifa. Vile vile, Wizara itasimamia uendeshaji wa mashauri ya jinai katika ngazi zote.

**55. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kuhifadhiwa, Wizara itakuza uwezo wake wa kushughulikia malalamiko yanayotokana na kukiukwa kwa haki za binadamu na misingi ya utawala bora; na pia itatoa elimu kwa wananchi. Hali kadhalika, Wizara itafanya utafiti utakaochangia kuimarishwa kwa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

**56. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarisha shughuli za usajili wa matukio muhimu ya binadamu, Wizara itasimamia utekelezaji wa mpango wa usajili wa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano katika mikoa ya Kanda ya Ziwa; kuhuisha viwango vya ada za usajili, udhamini na ufilisi; na kuanzisha mfumo wa malipo ya huduma hizo kwa njia ya kielektroniki.

**57. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itashiriki kikamilifu katika masuala ya kuleta utangamano wa kikanda; kufanya majadiliano yanayohusu mikataba ya kibiashara; na mikataba ya uhusiano wa kimataifa na kushiriki katika mikutano ya Kamati za uanachama wa mamlaka mbalimbali. Aidha, Wizara itawasilisha Bungeni miswada ya Sheria ya Msaada wa Kisheria; Sheria ya Kulinda Watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi. Vile vile, Wizara itaimarisha mfumo wa kielektroniki wa kupokea, kuchambua na kuhifadhi kumbukumbu za malalamiko.

**58. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaziimarisha taasisi za mafunzo zilizo chini yake, ambazo ni Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto ili ziweze kutoa huduma bora zaidi. Aidha katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara inakusudia kukamilisha miradi ya ujenzi wa majengo ya mahakama, ofisi na nyumba za watumishi; kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma na kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

**59. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itasimamia na kuratibu kazi za Kamati ya Kitaifa ya kuzuia mauaji ya kimbari; itawajengea uwezo waendesha mashtaka, mahakimu na maafisa ustawi wa jamii ili kusimamia vema mfumo wa utoaji haki kwa watoto kwa kuzingatia Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

**60. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nyingine zinazolenga kuweka mazingira mazuri ya utumishi, Wizara itaandaa mpango mahsus wa kuwashumia watumishi wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI na wale wenye magonjwa sugu yasiyoambukiza. Mpango huu unakusudia kuhakikisha kwamba watumishi wana ufahamu kuhusu afya zao na jinsi ya kujilinda.

## E. SHUKRANI

**61. Mheshimiwa Spika**, sasa naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia jitihada na mafanikio ya utekelezaji wa majukumu yetu. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa viongozi na watendaji wote wa Wizara kwa ushauri wao wa mara kwa mara toka nilipokabidhiwa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Katiba na Sheria; na kwa usimamizi makini wa majukumu ya Wizara yetu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Naibu Waziri

wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, Jaji Mkoo wa Tanzania; Mheshimiwa George M. Masaju, Mwanasheria Mkoo wa Serikali; Mheshimiwa Shaaban A. Lila, Jaji Kiongozi; Bibi Maimuna K. Tarishi, Katibu Mkoo, Wizara ya Katiba na Sheria; Bwana Hussein A. Kattanga, Mtendaji Mkoo wa Mahakama; Mheshimiwa Ignus P. Kitusi, Msajili Mkoo wa Mahakama; Bibi Sarah D. Mwaipopo, Kaimu Naibu Mwanasheria Mkoo wa Serikali; Mheshimiwa Jaji Aloysius K. Mujulizi, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; na Bwana Bahame Tom Nyanduga, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

**62. *Mheshimiwa Spika*,** pia niwashukuru Bwana Biswalo E. K. Mganga, Mkurugenzi wa Mashtaka; Mheshimiwa Jaji Dkt. Gerald A. M. Ndika, Mkoo wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo; Mheshimiwa Jaji Ferdinand L. K. Wambali, Mkoo wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto; Bibi Mary Massay, Katibu Mtendaji, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Bibi Agnes Mgeyekwa, Kaimu Katibu Mtendaji, Tume ya Kurekebisha Sheria; Bibi Emmy Hudson, Kaimu Mtendaji Mkoo, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini na Bibi Enzel W. Mtei, Katibu Msaidizi, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Wakurugenzi, watendaji na watumishi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria.

**63. *Mheshimiwa Spika*,** nitoe shukurani nyingi kwa Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, kwa miongozo na ushauri mbalimbali walioutoa kwetu wakati wote wa maandalizi ya makadirio ya bajeti ambayo leo hii ninaona fahari kuyawasilisha mbele ya Bunge lako tukufu.

**64. *Mheshimiwa Spika*,** nawashukuru pia wadau wa maendeleo ambao wameendelea kufanya kazi bega kwa bega na Serikali yetu kwa kutupatia ushauri na rasilimali fedha katika kuimarisha Sekta ya Sheria. Kwa namna ya pekee niwashukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la UN-WOMEN, Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA) na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Uingereza, (DfID).

#### **F. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016**

##### **Muhtasari wa Maombi ya Fedha**

**65. Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi 223,869,099,000 kwa ajili ya wizara na taasisi zake. Kati ya hizo Shilingi 197,806,773,000 ni kwa matumizi ya kawaida zikiwemo Shilingi 68,819,126,000 kwa ajili ya mishahara na Shilingi 128,987,647,000 kwa matumizi mengineyo. Fedha za Maendeleo ni Shilingi 26,062,326,000 kati ya hizo Shilingi 24,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 2,062,326,000 ni fedha za nje. Makadirio ya matumizi hayo kwa mafungu saba ya Wizara ni haya yafuatayo:-

|                 |   |  |   |                        |
|-----------------|---|--|---|------------------------|
| <b>Fungu 12</b> | - | Tume ya Utumishi wa Mahakama             | - | 4,003,456,000          |
| <b>Fungu 16</b> | - | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali    | - | 13,040,883,000         |
| <b>Fungu 35</b> | - | Divisheni ya Mashtaka                    | - | 21,545,505,000         |
| <b>Fungu 40</b> | - | Mfuko wa Mahakama                        | - | 158,487,513,000        |
| <b>Fungu 41</b> | - | Wizara ya Katiba na Sheria               | - | 16,141,825,000         |
| <b>Fungu 55</b> | - | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | - | 6,517,656,000          |
| <b>Fungu 59</b> | - | Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania      | - | 4,132,261,000          |
| <b>JUMLA</b>    |   |  |   | <b>223,869,099,000</b> |

### **Muhtasari wa Matumizi**

**66. Mheshimiwa Spika**, sasa naomba nitoe mchanganuo wa makadirio haya kwa kila fungu kama ifuatavyo:-

#### **(i) Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama**

|                               |              |     |                          |
|-------------------------------|--------------|-----|--------------------------|
| Matumizi ya Mishahara         | -            | Sh. | 668,916,000              |
| Matumizi Mengineyo            | -            | Sh. | 3,334,540,000            |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | -            | Sh. | 0                        |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje)   | -            | Sh. | 0                        |
|                               | <b>Jumla</b> | -   | <b>Sh. 4,003,456,000</b> |

**(ii) Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

|                               |          |            |                       |
|-------------------------------|----------|------------|-----------------------|
| Matumizi ya Mishahara         | -        | Sh.        | 3,832,615,000         |
| Matumizi Mengineyo            | -        | Sh.        | 7,908,268,000         |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | -        | Sh.        | 1,000,000,000         |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje)   | -        | Sh.        | 300,000,000           |
| <b>Jumla</b>                  | <b>-</b> | <b>Sh.</b> | <b>13,040,883,000</b> |

**(iii) Fungu 35: Divisheni ya Mashtaka**

|                               |          |            |                       |
|-------------------------------|----------|------------|-----------------------|
| Matumizi ya Mishahara         | -        | Sh.        | 9,365,978,000         |
| Matumizi Mengineyo            | -        | Sh.        | 11,836,643,000        |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | -        | Sh.        | 0                     |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje)   | -        | Sh.        | 342,884,000           |
| <b>Jumla</b>                  | <b>-</b> | <b>Sh.</b> | <b>21,545,505,000</b> |

**(iv) Fungu 40: Mfuko wa Mahakama**

|                               |          |            |                        |
|-------------------------------|----------|------------|------------------------|
| Matumizi ya Mishahara         | -        | Sh.        | 48,998,032,000         |
| Matumizi Mengineyo            | -        | Sh.        | 89,087,667,000         |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | -        | Sh.        | 20,000,000,000         |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje)   | -        | Sh.        | 401,814,000            |
| <b>Jumla</b>                  | <b>-</b> | <b>Sh.</b> | <b>158,487,513,000</b> |

**(v) Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria**

|                               |          |            |                       |
|-------------------------------|----------|------------|-----------------------|
| Matumizi ya Mishahara         | -        | Sh.        | 1,944,187,000         |
| Matumizi Mengineyo            | -        | Sh.        | 10,237,919,000        |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | -        | Sh.        | 3,000,000,000         |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje)   | -        | Sh.        | 959,719,000           |
| <b>Jumla</b>                  | <b>-</b> | <b>Sh.</b> | <b>16,141,825,000</b> |

**(vi) Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

|                       |   |     |               |
|-----------------------|---|-----|---------------|
| Matumizi ya Mishahara | - | Sh. | 2,779,581,000 |
| Matumizi Mengineyo    | - | Sh. | 3,680,166,000 |

|                               |   |            |                      |
|-------------------------------|---|------------|----------------------|
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - | Sh.        | 0                    |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje)   | - | Sh.        | 57,909,000           |
| <b>Jumla</b>                  | - | <b>Sh.</b> | <b>6,517,656,000</b> |

**(vii) Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria**

|                               |   |            |                      |
|-------------------------------|---|------------|----------------------|
| Matumizi ya Mishahara         | - | Sh.        | 1,229,817,000        |
| Matumizi Mengineyo            | - | Sh.        | 2,902,444,000        |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - | Sh.        | 0                    |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje)   | - | Sh.        | 0                    |
| <b>Jumla</b>                  | - | <b>Sh.</b> | <b>4,132,261,000</b> |

**Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali**

**67. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 17,023,933,750 ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

|              |            |     |                       |
|--------------|------------|-----|-----------------------|
| Fungu 12     | -          | Sh. | 0                     |
| Fungu 16     | -          | Sh. | 1,002,000             |
| Fungu 35     | -          | Sh. | 13,002,000            |
| Fungu 40     | -          | Sh. | 5,203,298,750         |
| Fungu 41     | -          | Sh. | 11,801,400,000        |
| Fungu 55     | -          | Sh. | 5,131,000             |
| Fungu 59     | -          | Sh. | 100,000               |
| <b>JUMLA</b> | <b>Sh.</b> |     | <b>17,023,933,750</b> |

**68. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**Kiambatisho A**

| MASHAURI YA DAWA ZA KULEVYA |                |                               |               |                |
|-----------------------------|----------------|-------------------------------|---------------|----------------|
| Mwaka                       | Aina ya madawa | Idadi ya Kesi Zilizofunguliwa | Uzito (gm)    | Thamani (Tsh)  |
| 2012                        | Heroine        | 14                            | 34,592        | 1,597,396,000  |
|                             | Cocaine        | 3                             | 11,970        | 592,275,000    |
|                             | Canabis        | 3                             | 47,114        | 56,800,000     |
|                             | Jumla Ndogo    | 20                            | 93,676        | 2,246,471,000  |
| 2013                        | Heroine        | 11                            | 16,487        | 732,615,000    |
|                             | Canabis        | 2                             | 170,420       | 276,000,000    |
|                             | Jumla Ndogo    | 13                            | 186,907       | 1,008,615,000  |
|                             |                |                               |               |                |
| 2014                        | Heroine        | 16                            | 256,707       | 12,377,812,000 |
|                             | Cocaine        | 8                             | 12,248        | 642,202,000    |
|                             | Canabis        | 1                             | 167           | 8,338,000      |
|                             | Jumla Ndogo    | 25                            | 269,122       | 13,028,352,000 |
| 2015                        | Heroine        | 1                             | Haujaainishwa | 51,144,000     |
|                             | Mengineyo      | 20                            | Haujaainishwa | Haijaainishwa  |
|                             | Jumla Ndogo    | 21                            |               | 51,144,000     |
|                             | Jumla Mkuu     | 79                            | 549,705       | 16,334,582,000 |

**Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama**

| <b>NA.</b> | <b>JINA LA MRADI</b>                                    | <b>HATUA ILIYOFIKIWA</b>  | <b>MAELEZO YA ZIADA</b>  |
|------------|---|---|--|
| 1.         | Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Tanzania                 | Zoezi la kusafisha kiwanja (site clearance) katika Mtaa wa Chimala limekamilika. Mchakato wa kumpata Mshauri elekezi (Consultant) imekamilika katika hatua zote na Mshauri kapatikana       | Majadiliano kabla ya kutia saini mkataba yanaendelea kwa ajili ya kuandaa michoro (architectural drawings), makisio ya gharama, makabrasha ya zabuni (tender documents) na kusimamia ujenzi. |
| 2.         | Ujenzi wa nyumba za Majaji katika Mkoa wa Dar es Salaam | Mshauri elekezi (TBA) anaendelea kufanya ukaguzi ( <i>Conditional survey</i> ) ili kupata mahitaji ya ukarabati (user requirements) nchi nzima, ili taratibu za ukarabati ziweze kuendelea. | Mahitaji hayo yatakuwa mwongozo wakati wa ujenzi wa nyumba za Majaji nchi nzima  |
| 3.         | Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 26                         | Mshauri elekezi <i>M/S PSM Architect</i> amekamilisha kufanya mapitio ya michoro, makisio ya gharama na rasimu ya makabrasha ya zabuni  | Rasimu za makabrasha ya zabuni zimehakikiwa na Mshauri anaandaa kitabu halisi cha kabrasha   |

|    |   |  |   |
|----|---|--|---|
| 4. | Ukarabati wa Mahakama Kuu katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara                                  | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Ukarabati wa Mahakama Kuu Dar es Salaam umekamilika katika hatua ya awali (practical completion)</li> <li>• Ukarabati wa Mahakama Kuu Mtwara unaendelea.</li> <li>• Mkandarasi alianza kazi ya ukarabati wa Mahakama Kuu Tanga mwezi Juni 2014 na ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2015.</li> </ul> | <p>Mradi huu utakuwa kwenye kipindi cha Matazamio kwa mwaka mmoja.</p> <p>Mradi utakamilika mwezi Februari na utakuwa kwenye kipindi cha matazamio kwa mwaka mmoja.</p> |
| 5. | Upanuzi katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama (Lushoto)   | Ujenzi wa kuta za mradi wa ujenzi wa bweni la wavulana umekamilika na maandalizi ya kupaua yanaendelea.  | Mradi huu ulisimama kutokana na matatizo ya kimkataba na majadiliano yanafanyika ili mradi uweze kuendelea na kukamilika mapema   |
| 6. | Ujenzi wa Mahakama za Wilaya Bunda, Bariadi, Bagamoyo, Bukombe, Kilindi, Nkasi, Makete, Hanang' na Kasulu | Mshauri elekezi (Chuo Cha Ardhi) amekamilisha kufanya mapitio ya michoro, makisio, na rasimu ya makabrasha ya zabuni   | Katika awamu ya II ya mkataba wake Mshauri huyu pia atasimamia kazi za ujenzi   |
| 7. | Ujenzi wa Mahakama Kuu Shinyanga (Awamu ya III)   | Mkandarasi M/S Masasi Construction yupo site na anaendelea na ukamilishaji wa mradi  | Mradi huu unatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa mwezi Juni 2015.  |

|     |  |   |   |
|-----|--|---|---|
| 8.  | Ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma, Mara, Lindi, Mtwara, Morogoro, Manyara na Singida na Upanuzi katika Mahakama Kuu Dodoma | Mshauri elekezi M/S Hab Consult Ltd amekamilisha na kuwasilisha rasimu michoro ya Architectural Drawings na Makisio | Michoro ya mwisho (detailed architectural and Structural) and services Drawings inakamilishwa sambamba na kuandaa makisio na rasimu ya makabrasha ya zabuni |
| 9.  | Ukarabati wa majengo ya mahakama katika maeneo mbalimbali hapa nchini  | Mshauri elekezi M/S Mekon Architect Ltd amekamilisha na kuwasilisha za rasimu michoro                               | Michoro ya mwisho (detailed architectural and Structural) and services Drawings inakamilishwa sambamba na kuandaa makisio na rasimu ya makabrasha ya zabuni |
| 10  | Ujenzi wa Mahakama Kuu Bukoba (Awamu ya III).  | Mkandarasi M/S Teki Enterprise amekamilisha ujenzi wa Mahakama kuu Bukoba awamu ya III                              | Mradi utakuwa kwenye kipindi cha matazamio kwa mwaka mmoja  |
| 11. | Ujenzi wa Mahakama ya mwanzo Magole Wilaya ya Kilosa Mkoani Morogoro.  | Mkandarasi M/S Eco Green Construction Co.Ltd amekamilisha ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Magole.                      | Mradi huu ultokana na mahakama iliyokuwepo kuathiriwa na mafuriko   |

**Kiambatisho C**

| JINA LA TAASISI                               | HALI YA WATUMISHI |         |                | MAOMBI YA AJIRA MPYA |           |           | MAFUNZO              |                      | KUPANDISHWA CHEO WATUMISHI |           | HALI YA UKIMWI (IDADI YA WATUMISHI) |           |
|---|-------------------|---------|----------------|----------------------|-----------|-----------|----------------------|----------------------|----------------------------|-----------|-------------------------------------|-----------|
|   | MAHITAJI          | WALIOPO | PUNGUFU/ZIA DA |                      | 2014/2015 | 2015/2016 | MUDA MREFU 2014/2015 | MUDA MFUPI 2014/2015 | 2014/2015                  | 2015/2016 | 2014/2015                           | 2015/2016 |
| Tume ya Utumishi wa Mahakama                  | 34                | 18      | -16            |                      | -         | 16        | 1                    | 1                    | -                          | -         | -                                   | -         |
| Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali         | 1,420             | 1,353   | -67            |                      | 352       | 67        | 34                   | 20                   | -                          | -         | -                                   | -         |
| Mahakama ya Tanzania                          | 23,816            | 5,684   | -18,132        | Mahakimu             | 57        | 8,357     | 551                  | 409                  | 685                        | 2,807     | 177                                 | 177       |
| Majaji  |                   |         |                | Majaji               | 22        |           |                      |                      |                            |           |                                     |           |
| Wizara ya Katiba na Sheria                    | 178               | 94      | 84             |                      | 2         | 31        | 6                    | 5                    | 15                         | 9         | -                                   | -         |
| Wakala wa Usajili, ufilisi na Udhamini (RITA) | 308               | 191     | -117           |                      | 6         | 42        | 14                   | 4                    | -                          | 106       | 3                                   | 3         |
| Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo  | 101               | 27      | -74            |                      | 19        | -         | -                    | 1                    | -                          | -         | -                                   | -         |
| Tume ya Kurekebisha Sheria                    | 67                | 55      | -12            |                      | -         | 5         | -                    | 2                    | 13                         | 12        | -                                   | -         |
| Haki za Binadamu na Utawala Bora              | 188               | 173     | 15             |                      | 2         | 4         | -                    | -                    | 35                         | 52        | 6                                   | 6         |
| JUMLA   | 26,112            | 7,595   | -18,319        |                      | 460       | 8,522     | 606                  | 442                  | 748                        | 2,986     | 186                                 | 186       |

**Kiambatisho D**

**MAKUSANYO YA MADUHULI YA SERIKALI KWA KIPINDI KINACHOANZIA  
JULAI, 2014-MACHI, 2015**

| FUNGU        | KIASI KILICHOPANGWA<br>KUKUSANYWA | KIASI<br>KILICHOKUSANYWA | ASILIMIA<br>(%) |
|--------------|-----------------------------------|--------------------------|-----------------|
| 16           | 4,502,000                         | 1,125,000                | 25%             |
| 35           | 17,103,000                        | 653,160                  | 4%              |
| 40           | 4,115,843,000                     | 3,634,757,047            | 88%             |
| 41           | 4,434,270,121                     | 4,944,881,914            | 112%            |
| 55           | 5,644,000                         | -                        | 0%              |
| <b>Jumla</b> | <b>8,577,362,121</b>              | <b>8,581,417,121</b>     | <b>100%</b>     |

**Kiambatisho E**

| MAENDELEO YA UDAHILI WA WANAFUNZI WA LAW SCHOOL MWAKA 2008 HADI 2015 |                  |                         |                          |       |        |                    |             |             |
|--|------------------|-------------------------|--------------------------|-------|--------|--------------------|-------------|-------------|
| Year   | Total Registered | Passed at First Sitting | Passed at Second Sitting | Total | Failed | Pending Supp Exams | Abscondment | Postponment |
| 2008   | 498              | 88                      | 235                      | 323   | 22     | 134                | 4           | 15          |
| 2009   | 717              | 103                     | 275                      | 378   | 87     | 215                | 5           | 32          |
| 2010   | 431              | 87                      | 194                      | 281   | 33     | 102                | 2           | 13          |
| 2011   | 599              | 163                     | 222                      | 385   | 41     | 156                | 0           | 17          |
| 2012   | 584              | 111                     | 204                      | 315   | 81     | 172                | 0           | 16          |
| 2013   | 668              | 136                     | 214                      | 350   | 31     | 274                | 0           | 13          |
| 2014   | 1160             | 77                      | 0                        | 77    | 29     | 265                | 0           | 15          |
| 2015   | 574              | 0                       | 0                        | 0     | 0      | 0                  | 0           | 0           |
| JUMLA  | 5231             | 765                     | 1344                     | 2109  | 324    | 1318               | 11          | 121         |